FRANSIS JORDAN NA UHUSIANO WAKE NA YESU KRISTO

Fr. Milton Zonta SDS

2015

Kazi ya kufanya tafakari ya kina kuhusu maada hii, ya kumwangalia Fransisi Jordani na uhusiano wake na Yesu Kristo, ni kazi ngumu, na wakati huohuo ni kazi yenye kufurahisha. Ili kuweza kuwa kwenye njia sahihi ya kuelewa uhusiano wa Mwanzilishi na Yesu Kristo ambaye ni kiini na penzi la maisha yake na kazi ya kitume, na pia mfano unaotuvuta katika namna yetu ya kuwa na kuishi katika ulimwengu wa leo – ningependa kupendekeza baadhi ya maswali ambayo tunaweza kuyatumia kama sehemu ya kuanzia safari yetu: Zipi ni tabia za msingi za utambuzi wa Fransisi Jordani kwa Yesu Kristo? Ni mabadiliko gani makubwa yaliyofanyika katika maisha ya Fransisi Jordani kama matokeo ya uhusiano wake na Yesu Kristo? Uzoefu gani wa Yesu Kristo katika maisha ya Fransisi Jordani ambayo unasababisha namna yake ya utume? Ninaamini kwamba maswali haya yatatusaidia kuishi utume wetu wa kisalvatoriani tukiwa na hali bora sana ya kiroho.

Nitakachojaribu kufanya, kwa namna moja, ni kuelezea uhusiano wa Fransisi Jordani na Yesu Kristo, kwa sababu haiwezekani kuongelea kuhusu maisha ya kiroho ya Mwanzilishi kama tukitenganisha na muungano wake hai, na Yesu. Mwanzoni tu mwa maisha yake, kama inavyotokea kwa watu mbalimbali, Fransisi Jordani alitosheka na imani ambayo inafundishwa katika kujua kuhusu Yesu Kristo, ni mkusanyiko wa maneno ya kiimani ambayo yamefundishwa juujuu bila kufuata kanuni muhimu zinazohusiana na imani thabiti. Hata hivyo, Fransisi Jordani aliikuza imani yake hatua kwa hatua ndani kabisa ya moyo wake. Kama tutakavyoona baadae, kuishi kwa bidii mtindo wa maisha wa Yesu wa Nazareti, namna yake ya kumwamini Baba, na mtazamo wake wa huruma kwa watu, kumbukumbu ya kiroho ya Fransisi Jordani inavutia sana. Safari yake inatusaidia kutambua hitaji la kujitahidi na kukomaa katika imani, hatua ambayo inamaanisha kuchunguza sana chanzo kikuu cha imani hii, kuzidi mila na desturi ambazo tumerithi.

"Mimi mwenyewe ninajitupa katika mikono yako, Mkombozi na Mwokozi. Pamoja nawe, kwa ajili yako, kupitia wewe na ndani yako, Nataka kuishi na kufa."

Baba Jordani: *Kumbukumbu ya Kiroho* I, 9:

15 Novemba 1875

Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani

Sura ya 3 Utangulizi

Habari juu ya maisha ya Fransisi Jordani inatupa mwangaza kwa sababu inakuza uhusiano wetu na Yesu ambaye kwa ufahamu mdogo kumhusu Yeye tumeupata kutoka katika ibada za mara kwa mara na habari za nadharia ambazo nyingi ni za kufirika. Imani ya mtindo huu haitoshi, tunahitaji uhusiano mkubwa na Yesu Kristo ambao unatokana na sala, tafakari ya neno la Mungu, namna yetu ya kujitoa sadaka kwake na pia majitoleo yetu kwa wengine kwa kupitia matendo ya huruma na muungano wetu na wale wanaoteseka. Kama tutakavyoona baadae, tutaongelea mitazamo ambayo tunatakiwa kuizoea, na tafakari ambazo tunatakiwa kuzichukua katika maisha yetu, mpaka tutakapofikia katika kina cha imani halisi ambacho mwanzilishi wetu alimwita Yesu Kristo "ee Bwana, ningetamani sana kama ningeweza kuugua kwa ajili ya kukupenda wewe na pia kuwasha moto huo kwa wengine. Je, ninaweza kuwa moto uwakao, ee Bwana, na tochi inayowaka

(SD III/20)?[1] Inawezekana swali letu la msingi kwa sasa ni: Tutaupata wapi moto uwakao sana ambao uliwaka kwa Fransisi Jordani? Je, Wasalvatoriani wanaume na wanawake wanafanya kazi kwa kudumisha uhusiano wao na Yesu Kristo? Wanatoa ushuhuda (sio kwa maneno tu) kwa ujumbe wa Yesu Kristo kama ni Habari Njema ya wokovu? Bila ya kuwa na uhusiano wa karibu na Yesu, ufuasi wetu unakuwa ni dini dhaifu. Papa Benedikto wa XVI alieleza jambo hili kwa uwazi: "Kuwa Mkristo hakutokani na uchaguzi wa kimaadili au fikra ya juu sana, bali kukabiliana na tukio ambalo linampa mtu uhai, upeo mpya na uelekeo wa uamuzi!"[2] Ninashawishika kwamba kurudi katika uhusiano huu hai na Yesu Kristo, na kuboresha roho yake, ambayo inakomboa uhai na kumfanya kuwa wa kibinadamu zaidi, ni kitu cha muhimu sana kwa upande wetu kwa sasa, kama matarajio ya kijana Fransisi Jordani. "Kwa mambo yote ufanyayo, sala zako, n.k. fanya katika Yesu, kupitia Yesu, pamoja na Yesu (…) Bila Yeye hautaweza kufanya chochote. Bila yeye chochote kile unachofanya ni kwa ajili ya nini?" SDI/125)

MANENO YA UTANGULIZI

Kabla ya kutafakari jinsi ya kuweka maisha yetu kwa Yesu Kristo pamoja na mtazamo wa Fransisi Jordani, ningependa kutoa baadhi ya maelezo ya utangulizi.

1: **Hatari ya kushikwa na ukale:** Tunaishi katika kipindi chenye mabadiliko makubwa ya kiutamaduni kila mahali, ambayo inaadhiri namna yetu ya maisha ambayo inahitaji kutoka kwetu mtazamo unaoona mbali kwa siku zijazo, bila kushikamana na mambo ya kale. Tunashikamana na ukale wakati tunatafuta uhusiano wetu wa nje na Fransisi Jordani kama muhusika fulani wa karne ya 19 ambaye ana historia nzuri ya maisha na aliyetuachia maandiko mazuri yanayomuhusu yeye. "Fransisi Jordani" huyu anapendwa na watu wachache tu. Hatari ya kumnukuu Mwanzilishi bila kutoa ufafanuzi wa maneno yake ili kuweza kuleta nguvu zake za uinjilishaji kwa kipindi chetu cha sasa inatuogofya popote tulipo. Hapa nitajaribu kuongelea kuhusu Fransisi Jordani anayevutia ambaye ni mfano wa maisha ya kiroho kwa ulimwengu wetu wa leo.

2: **Kisima cha maisha ya kiroho ya Baba Jordani** – katika miongo ya sasa tumefanya uchunguzi na tafsiri nyingi juu ya maisha na maandiko ya Fransisi Jordani. Lakini, sifahamu kazi yoyote ya kitaalamu kuhusu Yesu Kristo alivyoeleweka kupitia macho ya Fransisi Jordani. Katika kuitayarisha tafakari hii, niliweka mawazo yangu katika undani wa kiroho uliopo katika hifadhi ya maandiko yake ya kiroho bila kuangalia maandiko mengine. Kama tunavyofahamu, kitabu cha kumbukumbu cha kiroho cha Mwanzilishi si kitabu cha kufundishia. Kinaonyesha maisha yake ya ndani tu na kutuonyesha mifano mizuri, kama vile unyenyekevu wake, uaminifu kwa maongozi ya Mungu, ufukara wa kiinjili, tafakari na maisha ya kiibada. Wakati huohuo, inaonyesha majitoleo yake muhimu kwa kweli za kikristo. Kwa mfano, umuhimu wa Yesu Mwokozi, roho za mitume, upendo kwa Kanisa, majitoleo kwa Maria kama Msaidizi na Mlinzi, tafakari ya Neno la Mungu, na Sakramenti. Zaidi ya hayo, nadhani maandiko yake ya kiroho yanaonyesha tabia za kipekee. Kwa mfano, maisha yake ya kushikilia maadili mema, ustahimilivu, upatikanaji wake, roho ya jumuiya, na mapenzi ya kitume. Kwa hakika, kitabu cha kumbukumbu cha maisha ya Jordani ni utajiri halisi ambapo tunaweza kupata muendelezo, mvuto na nia za kitume za Baba Jordani.

---

[1] *Katika Sala hii, Mwanzilishi anamwomba Mwokozi amfanye kuwa shahidi wa mwanga, kama alivyofanya kwa mwombezi wake, Yohana Mbatizaji, ambaye "alikuwa taa inayowaka na kuangaza." (Yn 5:35).*

[2] *Barua ya Kichungaji "Deus Caritas Est" n 1 (2006); iliyotolewa Roma katika basilica la Mt. Petro, 25 Desemba.*

3: Kujaribu kutofautiana na Msingi Mpya:

Tafakari yangu haina lengo la kudharau kazi na fafanuzi ambazo wasalvatoriani wanaume na wanawake wamezifanya kwa kipindi hiki na kipindi cha nyuma. Lakini katika ulimwengu unaobadilika mara kwa mara hatuwezi tukakaa katika sehemu za kujidai za vitu vizuri au mambo mazuri ambayo tumefanikiwa mpaka sasa. Karama ya kisalvatoriani inakuwa kama ilivyo roho yake, wito wa kushiriki na kukuza wajibu wa kuishi, muda wa sasa. Kwa hiyo, tafakari ifuatayo ina lengo la kutoa ufafanuzi maalumu (kati ya fafanuzi nyingine) wa roho ya Fransisi Jordani, ambayo kila wakati ni kitu kipya. Utajiri wa maisha ya kiroho na mtazamo wa Baba Jordani kamwe hauchoshi. Changamoto iliyopo ni kutafuta lugha mpya ambayo itatuwezesha kubadili mpango ambao unaonekana hauna maana katika ulimwengu wa leo.[3] Wengi wanaweza kukubaliana na mimi kwamba kuna mambo mengi mazuri yanayofanyika sehemu mbalimbali, lakini kutokana na ubunifu wetu mdogo na ulio na mipaka, watu wachache tu wanathubutu kumfuata Yesu na kuchukua roho ya kitume ya Fransisi Jordani. Kwa hiyo basi, kama tunataka kuwa mashahidi wa wokovu leo na kushirikiana na Kanisa kubadili ulimwengu kuwa sehemu nzuri ya kuishi kwa wanadamu, ni lazima turudi katika mapendo ya kimungu na kitume ya mwanzilishi wetu. Kutafuta njia nyingine ya kuelezea maisha yetu ya kiroho si kazi rahisi, lakini ni lazima tujitahidi kama tunataka kuiondoa hali ya kutojali ambayo inatufanya kuwa watumwa wa ukale.

4: **Msingi wa maisha ya kiroho ya Baba Jordani**: Kama wanadamu wengine wowote wale, Fransisi Jordani alitengeneza maisha yake ya kiroho na kukua hatua kwa hatua kabla ya kuwa mfano wa uaminifu kwa Kristo kwa sasa na zamani. Lakini, tunaweza kulinganisha urithi wa maisha ya kiroho ya Baba Jordani na utajiri wa maisha ya kiroho yaliyotangulia (Wabenediktini, Wadominikani, Wafransiskani au Majesuiti) ambayo yalistawi katika maisha ya Kanisa kwa karne nyingi? Ingawa tunaweza kusema kwamba Fransisi Jordani hakutengeneza mfumo mpya wa maisha ya kiroho kwa mtindo uliozoeleka, kama zilivyo shule za kiroho zilizopo toka zamani, haina maana kwamba maisha yake ya kiroho yanakosa tabia yake utofauti na ya upekee. Nadhani tunaweza kusema kwamba kwa urithi wa maisha ya kiroho ya Fransisi Jordani tunatambua namna ya pekee ya kujitakatifuza na kutangaza upendo wa Mungu katika ujumla wake. Baba Mwanzilishi hakuanzisha asili ya maisha ya kiroho, lakini ninaamini alikuwa ni Baba wa kiroho ambaye alitupa namna mpya ya kusoma na kuishi Injili kwa wakati wake. Fransisi Jordani, zaidi ya hayo, alikuwa mtu wa sala ambaye alimpenda sana Yesu Kristo na alilipenda sana Neno la Mungu. Alikuwa ni mtume asiyechoka mwenye upendo wa dhati kwa Kanisa.

NJIA YA FRANSISI JORDANI KAMA MFUASI WA YESU

Uzoefu wa imani mara nyingi ulmaanisha kufuata njia, kama kielelezo cha fundisho la Abrahamu kinavyotueleza imani mara nyingi imekuwa ni safari, ahadi "katika tumaini dhidi ya tumaini aliloamini." Kama Mtk. Paulo anavyosema (Rom 4:18). Mkutano wa Fransisi Jordani na Yesu Kristo ni hadithi pia inayojifunua kwa hatua. Ni tukio la safari ya kiroho ambayo imepitia hatua mbalimbali, limepitia mabadiliko na, bila shaka, likaambatana na wasiwasi na magumu. Kama mara nyingi alivyoeleza katika kumbukumbu yake ya kiroho. Kwa mfano, baada ya Mkutano

[3] Labda tunahitaji lugha mpya badala ya kusema "kuokoa roho" tungeweza kusema "kuwaponya wagonjwa na waliojeruhiwa," badala ya kusema "maongozi ya kimungu" tungeweza kusema "kuona ulinzi wa Mungu na mapenzi yake ya kibaba," badala ya "kumbakumba" tungeweza kutumia "utume wa pamoja" na "bila kumbagua yeyote," n.k.

Mkuu wa Shirika wa Novemba 1902 aliandika: "Bwana! Mimi ni wako! Nisaidie, kamwe usiyaache majaribu ambayo yananimaliza." (SD II/41).

Ningependa kupendekeza kutofautisha hatua mbili za msingi kwa uzoefu wa Mwanzilishi wetu juu ya ufuasi kwa njia ya kufundisha zaidi kuliko njia ya kihistoria. Hatua ya kwanza inahusu maisha ya imani ambalo aliyapata kutoka tafakari za Kanisa kwa wakati huo, hasa kwa kupitia familia, jumuiya, ushuhuda wa baadhi ya watu na pia maisha ya mashahidi na ya watakatifu wengine. Kwa kipindi hiki, alisisitiza juu ya ibada ya majitoleo ya kikatoliki, ambayo yalijikita katika maisha na mafundisho ya Yesu Kristo. Aina hii ya majitoleo yanakubaliana na mtindo wa kanuni na usanifu wa imani, yanajionyesha katika matendo mbalimbali ya kiibada ambayo yanaboresha na kudumuisha majitoleo. Papa Paulo VI alisema ya kwamba ibada ya pamoja "inaonyesha kiu kwa ajili ya Mungu ambayo inaweza ikafahamika tu na watu fukara na wanyoofu."[4] Kama tutakavyoona mazoezi ya ibada ya Francisi Jodani yalimsaidia kupata roho imara ya ibada kwa njia ya majitoleo aliyoyachagua na kuyaishi kwa ajili ya karama na upendo kwa Yesu Kristu.

Zaidi ya hayo, ngoja, nionyeshe hatua ya pili ya habari ya imani ya Fransisi Jordani, ambayo kwa makusudi iliamuliwa kuingizwa tena katika maisha yake. Mwezi Oktoba 1877, kama tunavyofahamu, alijiunga na seminari ya jimbo ya Mtk. Petro huko Black Forest (Misitu Myeusi). Mazoezi ya kiroho ya Mtk. Ignasius wa Loyola yalikuwa ni ya muhimu sana kwa mwaka wake wa mwisho wa malezi. Mwanzilishi kijana alijikita sana kujifunza juu ya wataalamu wakuu wa maisha ya kiroho, hasa Andre-Jean-Marie Hamon (1795 – 1874),[5] na Mjesuiti Luis de la Puente (1554 – 1624) na Paolo Seguezi (1653 – 1713). Kusoma huku kwa bidii, ukiongezea na mazoezi yake ya tafakari, kulimsaidia kuwa na uhusiano wa pekee na wa karibu sana na Yesu. Kwa kweli, aliboresha sana maisha yake ya kiroho kama alivyojaliwa, ambayo yaliboresha urafiki wake wa karibu na Yesu Kristo, ambapo baada tu ya kupewa daraja ya ushemasi aliandika "Katika masomo yako soma sana juu ya kweli za kiteolojia, hasa kwa njia ya kitafakari. Vipimo nusu havina faida sana" (SD I/126). Katika kipindi hiki cha malezi ya juu, ukimya na utambuzi tunaona picha ya mwanzo ya "Jamii ya kikatoliki ya makleri na wafanyakazi katika shamba la Bwana kutoka mataifa yote" (SD I/124). Ni vigumu sana kueleza jambo hili kwa uhakika mkuu, bali nakiona kipindi hiki kama upeo mpya, ambapo Fransisi Jordani alikomaa katika ukaribu wake na Yesu, katika kumjua, kumpenda na kumfuata Yesu kwa uhakika. Kwa kifupi, umuhimu huu wa Yesu Kristo katika maisha ya Jordani ilikuwa ni njia iliyompeleka katika ukomavu na ukamilifu kama mfuasi na mtume wa Ufalme.

Ninawaalika sasa tuangalie kwa undani hatua hizi mbili za safari ya kiroho za Fransisi Jordani kwa kweli ilikuwa ni vipindi viwili ambavyo vipo katika mchakato ulio sawa, ambao hutusaidia kuelewa uzoefu wake wa imani na uhakika mkuu kama mfuasi wa Kristo na shuhuda wa wokovu.

---

[4] *Rejea Barua ya Kitume Evangelii Nuntiandi, 48*

[5] Mteolojia na mwandishi ambaye alimvuta sana Mwanzilishi wetu, ambaye alikuwa na maandiko yake muhimu: *Maisha ya Mtk. Fransis wa Sale na Sala na tafakari ya kila siku na kwa ajili ya mapumziko makubwa ya mwaka, (vitabu 3).*

1. Uzoefu wa mwanzilishi wa kumwamini Yesu Kristo

Kama tunavyofahamu, Fransisi Jordani alikuwa katika mazingira ya kidini na kiroho ya karne ya 19. Katika kipindi hiki, kulikuwa na mapinduzi makubwa ya kijamii, kisiasa na kiutamaduni ambayo yalizima uwezo na nguvu ya kufanya kazi kwa Kanisa Katoliki. Katika kupambana na hali hii, kulikuwa na jitihada za kuimarisha uwezo wake wa kiroho kwa kuanzisha mashirika mbalimbali ya kitawa. Pongezi kwa ushuhuda wa watakatifu mbalimbali na pia uboreshaji wa sala mbalimbali ya pamoja.

Moja ya mambo yaliyojitokeza katika mambo ya kiroho ya kikristo kwa kipindi hiki ilikuwa ni Ibada ya Kuheshimu Moyo Mtk. Wa Yesu. Hii ilisababisha karibu mashirika yote ya kitawa kwa kipindi hiki cha karne ya 19 yalikuwa na kitu kinachohusiana na Moyo Mtk. Wa Yesu ambayo ilisambaa sana kwa ibada ya pamoja.[6] Maendeleo haya ya ibada ya pamoja kwa Moyo Mtk. wa Yesu yalimvutia Fransisi Jordan; ingawa hakuna ushahidi wa ibada ya kuzidi iliyoonekana kwake. Kinyume chake, alitimiza njia hizi kuboresha maisha yake ya kiroho. Kwa mfano, alipokuwa akisoma katika seminari ya Mtk. Petro huko Black Forest, aliandika katika kumbukumbu yake ya kiroho "Mara zote hakikisha unakuwa na picha ya Moyo Mtk. wa Yesu, ambayo ipo chumbani kwako kwa ajili ya kuiabudu (veneration) kuiheshimu" (SDI/81) Alipoandika kanuni za kwanza za Shirika, mwaka 1880, aliitolea kazi yake ya kitume kwa moyo Mtk. wa Yesu.[7] Zaidi ya hayo, alipoanza kuchapisha jarida lake "*Missionary"* (mmisionari), jarida lake lilikuwa na picha ya Moyo Mtk. ikifuatiwa na sentensi ifuatayo "Moyo wangu mpendwa wa Yesu, niwezeshe niweze kukupenda zaidi mara zote." Kinachofurahisha zaidi ni mchoro wa mwanzo wa muhuri wa Shirika. Ulikuwa na picha ya Moyo Mtk. wa Yesu. Kwa hiyo, hatuwezi kutenganisha uwepo wa upendo wa Moyo Mtk. wa Yesu na maisha ya kiroho ya Fransisi Jordani, kwa sababu kila wakati ulimvutia, na ninadhani ilikuwa ni hatua ya mtazamo wake wa fikara na utayari wake wa kudumu kwa kazi ya kitume.

Ni lazima pia tuonyeshe kwamba majitoleo kwa Moyo wa Kristo (Moyo Mtk.) uliambatana na majitoleo maalumu kwa Ekaristi na mateso na kifo cha Yesu. Kwa ujumla mambo haya mawili muhimu ya ibada ya pamoja ambayo, pamoja na majitoleo kwa Bikira Maria, yalikuwa ni nguzo kuu tatu za maisha ya kiroho ya Fransisi Jordani. Miaka yote ambazo ameitumia katika seminari ya Mtk. Petro, alifafanua katika maandiko yake ya kiroho: "I. Ekaristi Takatif, II. Madonda Matano ya Bwana Wetu Yesu Kristo, III. Mtk. Sana Bikira Maria, Mama yangu" (SD I/126). Zaidi ya hayo, kama mtu mzima, mwezi Septemba, 1905, alionyesha tena mambo haya matatu kwa majitoleo yake: "Ekaristi Takatifu – Msalaba – Mama wa Mungu." (SD II/92).

Ninapoendelea na tafakari hii, ninaamini kwamba sasa ni muda mwafaka wa kuonyesha uhusiano wa Mwanzilishi na Yesu Kristo kupitia kujitoa kwake kwa Ekaristi na hadithi za mateso. Mambo haya yalimsaidia Jordani kupambana na magumu ya mara kwa mara. (Katika tafakari na tafakari

---

[6] Mwaka 1856 Papa Pio wa IX, baada ya kusikiliza maoni ya maaskofu mbalimbali, alifanya Sikukuu ya Moyo Mtakatifu wa Yesu kuwa kwa Kanisa zima. Lilikuwa ni jambo la pekee. Kutoka pale, kama hati ya liturujia inavyosema, "*Ibada za Moyo Mtk. Wa Yesu, kama mto unaofurika, zimeondoa vipingamizi vyote na kusambaa ulimwenguni kote."* Kipindi cha upapa wa Leo XIII, uzuri wa ibada ya Moyo Mtk. Uliboreshwa. Pongezi kwa kuchapwa kwa barua ya kichungaji Annum Sacrum (Mei 25, 1899). Katika barua hii, Baba mtk. aliamua kuwaweka wakfu watu kwa Moyo Mtk. Wa Yesu *"katika Moyo huo Mtk. lazima kuweka matumaini yetu yote na kutoka huo wokovu wa watu utafutwe kwa uhakika"* (Rej. Gonzalez, Manuel Revvelta, SJ. *Evolucion Historica dela devocion a Corazon de Jesus en Espana).*

[7] *"Jamii Fundishi ya Kitume inawekwa Wakfu kwa Moyo Mtakatifu wa Yesu" (Rejea ATS, kanuni, 16).*

zetu kwa neno la Mungu kwa mwanga wa hali yetu na tunapoadhimisha masakramenti, tunaweka kwa pamoja sala na matendo yetu. Kwa kufanya hivyo, tunajitahidi kuishi wito wetu kwenye utakatifu na kuwafanya wengine watende hivyo. Katiba # 11)

A) Majitoleo ya Mwanzilishi kwa Ekaristi – Bila shaka yoyote, uwepo wa Yesu katika Ekaristi na pia katika tabernakulo ilikuwa ni msingi na upendo wa maisha ya Baba Jodani. Mtu aliyemvutia sana katika jambo hili alikuwa ni Padre Nikolaus Gihr (1839 – 1924) ambaye alikuwa ni Baba yake wa Kiroho katika Seminari ya Mtk. Petro ambaye kazi yake mashuhuri ilichapishwa mwaka 1877, Sadaka Takatifu ya Misa. Alimsaidia Fransisi Jordani kuboresha mtizamo wa muungano wake na Yesu katika Ekaristi Takatifu. Kati ya malengo ya sala zake za kila siku, tunaona tamaa yake ya kumtembelea Yesu katika Sakramenti ya Ekaristi mara nyingi. Alipokuwa mseminari, aliandika "Mtembelee Yesu katika Sakramenti ya Ekaristi walau mara moja kwa siku" (SD I/90 na SDI/140). Kama mtu mzima, baada ya mafungo ya kiroho, aliandika tena: "Kaa peke yako kila mara karibu na tabernakulo ukiwa umejitenga na mambo yote" (SD II/92). Kwa Fransisi Jordani, wakati wa sala mbele ya Ekaristi Takatifu ilikuwa ni fursa nzuri kuonyesha shukrani kwa Mwokozi wake na kumwambia ananipenda mno kiasi gani. Nathubutu kusema kwamba Yesu alikuwa mzima na alikuwepo muda huu kama Yesu alivyokuwepo kwa mitume, na kwa hivyo Fransisi Jordani aliweka katika mikono ya Yesu maamuzi yote, matarajio na matendo ya maisha yake.

Katika Tafakari na Tafakuri zetu za ndani kwa neno la Mungu kwa mwanga wa hali zetu na tunapoadhimisha Masakramenti, tunaweka kwa pamoja sala na matendo yetu. Kwa kufanya hivyo, tunajitahidi kuishi wito wetu kwenye utakatifu wa kuwafanya wengine watende hivyo.

Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani # 11

Kwa Fransisi Jordani, jambo la pekee katika majitoleo haya ilikuwa ni mazoea yake ya kutumia muda katika tafakari na utambuzi wa wito baada ya Misa ya Jumapili. Kuna maandishi mbalimbali katika kitabu chake cha kumbukumbu inayoonyesha muda wake maalumu wa muungano wake na Kristo, kwa mfano: "Baada ya adhimisho la Sadaka Takatifu ya Misa kamilisha kazi hiyo kwa utukufu wa Mungu na wokovu wa wanadamu. Ee Yesu, ee Mtk. mwenye harufu nzuri – ndani yangu mimi mdhambi, Ee Mpendwa Wangu!" (SD I/149). Mwezi Machi, tarehe 05, 1879 aliandika tena, "Baada ya Misa Takatifu, nafikiri kama nilivyofanya muda mwingine baada ya Komunyo Takatifu."(SD/151+) Pia Mei 21, 1880 "Mara nyingine tena baada ya Adhimisho la Misa Takatifu shangwe kubwa na furaha" (SD I/156*). Rejea hizi ni uthibitisho wa jinsi muungano wake na Komunyo Takatifu ulihuisha nguvu zake na kustawisha maisha yake ya kiroho kama kweli "Mkate wa Uzima" na "Chakula cha malaika" (SD I/8). Katika njia yake kama mfuasi wa Yesu, kama alivyotambua msingi wa kazi yake ya kitume, nyakati hizi za ukaribu na "Mpendwa wake" inakuwa ni chanzo cha mwanga, nguvu na faraja ya Mwanzilishi wetu.

B) Majitoleo kwa mateso ya Yesu – Fransisi Jordani alifahamu vizuri sana sentensi ya Mtk. Thomasi wa Aquino"Mateso ya Kristo yanatosha kutumika kama mfano na mwongozo wa maisha yetu."[8] Kwa kweli, kutafakari mateso na kifo cha Yesu Kristo ilikuwa ni kitu kinachojitokeza mara

[8] *Saint Thomas Aquinas – Kuhusu Imani, 6 I c*

kwa mara katika maisha ya kiroho ya Mwanzilishi wetu na utume wake tangu alipokuwa kijana. Fransisi Jordani aliuishi mwungano wa karibu sana na Mwokozi Msulubiwa na akachukua lengo hili "kila wakati beba msalaba wako!" (SD I/93) Kama tunavyofahamu, Francisi Jordani alikuwa na msalaba chumbani kwake pamoja na picha ya Mama Mwenye Huzuni ambaye alimwomba na kumpenda sana. Bila shaka yoyote ile, aliutazama msalaba na Mama wa Mateso kila mara na kusema sala fupi, kwa mfano: "Ee Yesu, uliyeteseka kwa ajili yangu, Ee Baba, Ee uliye kila kitu changu. Jambo moja tu ninalokuomba, jambo moja tu, Bwana Mwenyezi, ninalotafuta! Ninatamani sana ningemwokoa kila mmoja (SDI/140). Alama mbalimbali kama hizi zinaonyesha kwamba Fransisi Jordani alitafuta utakatifu kwa njia ya mateso. Na kumtafakari Yesu msulibiwa ilikuwa ni chanzo cha tamaa yake ya kumwokoa kila mmoja."

Zaidi ya lugha ya maneno, Fransisi Jordani alijielezea kwa kutumia ishara kwa hiari na kwa unyoofu, ambayo inaonyesha tabia ya uchaji wa wazi hata siku ya leo. Anatuonyesha mfano wa pekee wa mtindo huu wa ibada pale alipotembelea kaburi takatifu la Kristo mwezi Machi, 1880. "Kitabu hiki kiliwekwa juu ya kaburi la Bwana wetu Yesu Kristo, juu ya mlima wa Kalvari, juu ya altare ya Bwana wetu Msulubiwa, Yesu Kristo, na juu ya altare ya Mama yetu, Maria wa Mateso, na pia kwenye sehemu ambapo msalaba mtk. ulisimama na pale ambapo Mkombozi wa ulimwengu alikufa" (SD I/155*). Zaidi ya majitoleo yake binafsi, ishara hii inaonyesha pia jinsi Mwanzilishi alivyoguswa kwamba mateso ya msalaba yanaonyesha njia yake kabla ya kutimiza kazi ya kitume ambayo ameifunua kama mwaliko.

Zaidi ya hayo, kwa kutafakari maumivu ya Kristo alipata msaada aliohitaji kuyashinda magumu yake mwenyewe: kusali vizuri na kuendelea mbele kwenye utakatifu wa rohoni. Moja kati ya malengo yake muhimu sana ya kiroho wakati akisoma seminarini yalikuwa ni: "Yaruhusu mateso ya Bwana wetu Yesu Kristo yawe lengo la kupenda kusumbuka na Bwana wetu Yesu Kristo (SD I/123), "tafakari mara kwa mara juu ya mateso ya Bwana wetu Yesu Kristo!" (SD I/144). Baada ya hapa, kama Padre Mtawa, aliandika jambo hili kuonyesha maisha ya Kristo ya msalaba aliyoishi. "Vumilia katika mateso na katika msalaba, ah, vumilia sana na kwa ushujaa. Jipe moyo, mwanangu! Niangalie Mimi msalabani! Ah, vumilia, Ah, vumilia kwa utii! Kumbatia msalaba na uubusu. Pasaka asubuhi inakuja mara!" (SD I/175) Kwa kweli, majitoleo ya kufanya tafakari juu ya mateso na kifo cha yesu kilikuwa ni moja ya mambo muhimu ya chanzo cha maisha ya kiroho yaliyomhusu Mwanzilishi wetu kuishi – kwa undani, kwa makini na mara zote – ambacho Mwokozi wa ulimwengu alifanya kwa ajili ya wanadamu. Fransisi Jordani aliona mateso ya Yesu kama njia mwafaka kufikia ufukara wa ndani, uliotegemea kujitoa kwa wengine kwa kujitoa wenyewe ili tumfuate Yesu Kristo kwa ukamilifu.

"Ushuhuda wa Baba Jordani na Mwenyeheri Maria wa Mitume unatusukuma…kukumbati a msalaba kwa ajili ya utume wetu…"

Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani # 12

2. Uzoefu wa Mwanzilishi wa kuamini kama Yesu alivyofanya.

Zaidi ya njia yake ya kumwungama Yesu kama Kristo kwa njia ya uchaji wa wazi, ninaamini Fransisi Jordani alikuwa ni mwenye imani kubwa na imara, yaani kuishi imani alivyoishi Yesu katika kipimo hiki cha kiroho, sio swala la "kuamini katika Yesu". Mazoezi ya kiroho ya kiignasi yalimsaidia kuboresha uhusiano wa karibu na Yesu Kristo. Njia ya kiroho iliyotungwa na Inyasi wa Loyola ilimwunganisha na Yesu Kristo kwa karibu na ilisaidia kukuza nafasi yake ya kuwa mtume kwa ajili ya huduma ya Kanisa.

Kwa hiyo, ningependa sasa "kusoma" pamoja nanyi njia ya Fransisi Jordani ya makuzi ya kiroho kwa mwanga wa uzoefu kamili wa Yesu wa Nazareti ambayo ni fumbo la juu na kueneza utume. Ninaamini juu ya misingi miwili ya desturi za Yesu kutoa mwanga wa mmisionari ambao tunaupata kutoka kwa Mwanzilishi. "Fundisheni mataifa yote (…..) kumjua Mungu wa kweli na Yule ambaye amemtuma, Yesu Kristo (….) Nendeni, na kwa ustahimilivu maneno yote ya uzima kwa watu."[9] Zoezi la kuleta vitu hivi viwili pamoja – ili kumjua Mungu na kutangaza habari njema za Yesu – ilimpeleka Fransisi Jordani katika ukomavu na pia ilikuwa ni ufupisho wa karama yake na muelekeo wake wa msingi kama Mmisionari.

2.1. Ufuasi ukivutiwa na fumbo la Yesu ("Abba"). Yesu wa Nazareti alimwita Mungu kwa neno "Abba" Baba? ambayo kwa mazingira ya familia ya kiyahudi ilionesha upendo, ukaribu na uaminifu kwa mtoto mdogo kwa baba yake. Vianzo vyote vinaonyesha kwamba Yesu alimwona Mungu yupo karibu naye, Baba Mpendwa ambaye anamwangalia kila mtu kwa huruma na mapendo makuu. Uzoefu huu wa kiroho ulionyesha utayari uhuru wa Yesu kufanya kazi kwa ajili ya maisha ya kiutu zaidi kwa kila mmoja, kuanzia kwa wale wasio na bahati.

Kutokana na maelezo haya, ningeweza kukiri fumbo la uzoefu wa kimungu, wa kutimiza na ya wa kiutu wa Yesu kwa Mwanzilishi wetu. Kupenda kumjua Yesu Kristo kama msingi wa maarifa yote ilikuwa ni jambo lilioujaza moyo wa Baba Jordani na kuupa uhai wake wote. Kwa kupitia mfano wake na mafundisho yake, Mwanzilishi wetu, ambaye maisha yake yalijengeka katika uhusiano huu na Yesu Kristo, alituita kuimarisha mwungano huo kama umuhimu wa kwanza na wa pekee katika maisha yetu wenyewe. Ili kuelewa vizuri muono huu wa sala ya Yesu na maisha yake ya kiroho ambayo alikuwa akiishi Fransisi Jordani, ningependa kuelezea mambo matatu:

a) **Elimu ya Mwokozi inayotoka katika Biblia** – Toka pale alipokuwa mwanafunzi, Fransisi Jordani alijitahidi sana kumjua Yesu Kristo kwa kutafakari maandiko matakatifu. Biblia ilikuwa ni kitabu cha maisha yake. Kwa kupitia neno la Mungu, alianza kuwa karibu na Yesu na aliyaweka maisha yake katika ujumbe wa Injili. Ni ukweli usioelezeka kwamba "kumjua mtu" kwa njia ya biblia haimaanishi uelewa wa akili lakini pia uzoefu wa uwepo wa mtu katika maisha yetu.

Zaidi ya hayo, alifanya jitihada ya kumjua Kristo. Ilimpeleka katika kuboresha muungano wake na Yeye. Kusikia, kutafakari, kuishi na kuadhimisha neno la Mungu ilikuwa ni jambo la muhimu sana katika maisha yake kwa sababu kama Mtk. Yeronimo alivyosema: "Ujinga wa Maandiko Matakatifu ni kutomjua Kristo (kutojua Maandiko Mtk. ni kutomjua Kristo.)" Ningependelea kuonyesha kwamba Fransisi Jordani alichukua maamuzi mazuri sana hasa kutoka kwa Mtk. Jeronimo. Tunafurahi kukuta nukuu aliyoikuta katika kitabu "Soma Maandiko Matakatifu mara nyingi. Zaidi sana, usiruhusu Maandiko Matakatifu yakupotee….Usingizi ukukute wakati umeshika Biblia na ukurasa Mtakatifu ukisaidia kichwa chako kinachoinama." (SD I/145) Nadhani tafakari hizi zinatosha kutuonyesha jinsi maandiko mtk. yalivyomwangaza na kuongoza hatua za Baba Jordani. Katika maisha ya kiroho ya Baba Jordani, tunaona kwamba, maandiko matakatifu hayana mbadala katika ustawi tunaouhitaji ili kufikia maarifa ya kiundani ya Yesu Kristo, Neno la Mungu aliyetwaa mwili. Ni neno la Mungu linaloishi ambalo Wasalvatoriani wanaume na wanawake wanalileta duniani kupita maneno na matendo yao.[10]

---

[9] *Angalia Sheria 1884.*

[10] Hitimisho la Hati ya Apareida (2007) imeelezea vizuri sana "kumjua Kristo ina maana gani kwetu.*" Kumjua Yesu ni zawadi nzuri sana ambayo mtu yeyote anaweza kuipata. Kwamba tumekutana naye ni tukio zuri sana lililotukia katika maisha yetu, na kumfanya ajulikane kwa maneno yetu na matendo yetu ya furaha" (29).*

b) **Kumwamini Mungu kama jambo la msingi** – kama tunavyofahamu, uaminifu umetawala katika Biblia daima. Uaminifu wa Yesu katika mapenzi ya kweli kwa Baba yalikuwa ya hali ya juu. Kwa jinsi hiyohiyo, huu ulikuwa ni mtazamo wa msingi kwa Fransisi Jordani. Aliyasikia maneno ya Yesu kama mwaliko binafsi: "Usiruhusu moyo wako kusumbuliwa. Mwamini Mungu. Niamini na mimi pia." (Yn 14:1). Katika maisha yake yote, mtazamo wa mwanzilishi ulionyesha kwamba Baba wa Yesu alikuwa anamsaidia kila wakati kama ni chanzo na hekima ya maisha. Tunavutiwa kila wakati kwa jinsi Mwanzilishi wetu alivyojitoa katika kualika nguvu ya upendo wa Mungu katika moyo wake. Kama sala ifuatayo inavyoonyesha, kumwamini Mungu haimaanishi kutomjali au kutohusika nae, bali ni chanzo kisicho cha kawaida cha kumsaidia "Wewe, Bwana, umekuwa tumaini langu, nguvu yangu, msingi wangu. Wewe ni msaada wangu. Wewe ni mlinzi wangu imara. Kwako ninaweka matumaini yangu na uaminifu wangu!" (SD II/64). Kama sala baada ya Komunyo, kuna wakati aliandika kwamba "katika mikono yako, eh Mwokozi na Mkombozi wangu, ninajirusha kwako, pamoja nawe, kwa ajili yako, kupitia kwako, na katika wewe ningetamani kuishi na kufa" (SD I/9). Baada ya kufikia ukomavu wa kiroho, pale kila kitu kwenye maisha kilivyoenda kama inavyotarajiwa, aliandika usemi huu: "Tumia funguo hizi. Mwamini Mungu na pia sala!" (SD II/66). Tuuruhusu uaminifu wetu usioyumba katika maongozi ya upendo wa Mungu yanayotuongoza ni sehemu ya muhimu sana ya maisha yetu ya kiroho ya kisalvatoriani.

c) Kutumia muda peke yako ukiwa na Mungu – Fransisi Jordani aliutumia kwa uangalifu sana muda wa mawasiliano yake na Mungu kwa hali ya upweke na ukimya. Watu wengi walimkumbuka kama mtu aliyekuwa akipenda kusali mara nyingi na "…kuwa katika muungano na umoja wa karibu sana na Yesu ambaye bila yeye huwezi kufanya chochote" (SD I/134). Tungependa kusoma maandishi yake ya kiroho tukimuona Mwanzilishi binafsi anayesali. Kumbukumbu yake ya maisha ya kiroho inaonyesha muda wake wa karibu sana akiwa peke yake pamoja na Yeye ambaye tunajua anatupenda upeo. Maandiko yake mara nyingi yalikuwa yanaonesha alivyokuwa anajisikia mbele ya "Wewe," ambaye kila wakati alikuwa na uwezo wa kuongea naye, akiwa pamoja naye, hakuwahi kujisikia mpweke hata mara moja. Maelezo ya upendo aliyotumia katika maandiko yake, kana kwamba alikuwa pamoja na mtu ambaye alikuwa ameungana naye kwa upendo mkuu, unaogusa sana. "Mpendwa wangu" (SD I/107). "Mpendwa wa moyo wangu" (SD I/143); "Mpenzi wa roho yangu" (SD I/144); "Ee Yesu wangu, Mwana wa Mungu aliye hai, mimi ni wako maisha yote! Kuteseka kwa ajili yake! Yote kwa ajili yako! Ee muda wa neema ya pekee!" (SD II/86). Nguvu ya kiroho inayomiminika kutoka katika sala na tafakari ya Baba Jordani ilikuwa na nguvu sana ambapo hakuna aliyeweza kumtenganisha na njia hii. Kutokana na muono wangu, hii haikuwa sehemu tu ya maisha yake pekee lakini pia moja ya urithi muhimu aliotuachia: nguvu kubwa ya kubadili kila kitu katika maisha yetu ambayo tunayapata kutoka maongezi yetu ya mara kwa mara peke yetu pamoja na Yesu, Bwana na Mwokozi wetu.

2.2 Ufuasi unaotegemea uzoefu wa Yesu wa kutangaza Habari Njema (Ufalme wa Mungu) - Vyanzo vyote vinaonyesha kwamba Yesu alianza kazi yake ya kuokoa si kwa kujiongelea Yeye Mwenyewe au kuhusu Mungu tu, bali kutangaza Ufalme wa Mungu kama tukio la Habari Njema. Ufalme wa Mungu ulikuwa, bila tatizo lolote, kiini cha mahubiri ya Yesu, ushawishi wake, na mapenzi yaliyomsukuma katika shughuli zake zote. Ufalme wa Mungu ni ufunguo wa kuelewa hali aliyoitoa katika maisha yake. Huu ni mtazamo chanya wa kuelewa ujumbe kuhusu Mungu ambaye yupo hapa kwa ajili ya kutafuta maisha ya furaha kwa watu wote, akijitahidi kujaza ulimwengu mzima kwa huruma yake. Kwa ujumbe huu kuhusu ujio wa Ufalme wa Mungu, Yesu anawakaribisha watu wote kubadili mioyo yao na namna yao ya kuangalia ukweli.

Wakati tunapoangalia maisha ya kichungaji ya Fransisi Yordani, ni rahisi kutambua nia yake ya pekee ya kufika sehemu za mbali sana, kutoka nje na kukutana na watu wote bila kumbagua hata mmoja. Kutokana na mwanzilishi, kitu kikubwa ambacho kila mmoja wetu ataweza kufanya katika maisha yake ni kuwapa watu nafasi ya kumtafuta Yesu na ujumbe wake wa kuokoa. Kwa lengo hili, Mwanzilishi alianzisha na kutuma makundi ya wamisionari kama "nguvu kazi ya kitume" kuweka mbegu ya Injili mioyoni mwa watu. Tamaa yake kuu ilikuwa ni "kuokoa roho," ambayo kwa lugha ya kisasa alimaanisha kumwokoa binadamu mzima na kila mmoja. Kwa maneno mengine, alipenda kujitolea maisha yake yote kwa ajili ya wengine, na kufanya bidii ili watu wengi zaidi inavyowezekana wawe na uzima tele.

Ili kuelewa vema mwendelezo wa utume wa Yesu ambaye alijitahidi kumfikia kila mmoja, kutafsiri kwa miono wa Fransisi Jordani, ningependa kuongelea vipengele vitatu:

a) *Moyo wa Kitume na Utambuzi wa Kitume* – Kuna moyo imara wa utume katika maisha ya Fransisi Jordani kwa kufuata mfano na maelekezo ya maneno ya Paulo "Ole wangu mimi, ee Bwana, kama sitakufanya ufahamike na wote!" (SD II/2). Kutangaza Injili ilikuwa ni wajibu wake. Wajibu uliomgharimu maisha yake yote. Kwa sababu hii Mwanzilishi alijaribu kila wakati kuweka akilini mwake ushuhuda wa wanaume na wanawake ambao, kutokana na mapendo yao kwa Kristo, walikuwa na mapendo kwa binadamu, kwa ulimwengu na zaidi sana kwa wale wanaoteseka. Kwa kufuata mfano wa mashahidi wengi wa Yesu Kristo, Fransisi Jordani alikuwa mtu anayejitoa, mwenye upendo, na mtu mwenye shauku ambaye hata mara moja hakujiruhusu kuwa na mapumziko. Kwa kuangaziwa na mwanga wa Mtume Paulo, alielezea kazi yake ya maisha kama ifuatavyo: "Kuwa mtume wa kweli wa Yesu Kristo, usipumzike mpaka umepeleka neno la Mungu pande zote za dunia, uwe mjumbe wa kweli wa Yeye aliye juu!" (SDI/182). Siku alizokuwa anajiandaa kwa Sakramenti ya Upadrisho, hitaji hili la moyo wake lilionekana wazi. "Ee mitume watakatifu, mlioenea ulimwenguni kote kuwahubiria wote! Ee shauku kubwa…" (SD I/138) Jitihada hizi na upendo huu wa Baba Jordani, ambao unatafakari juu ya utume wa mitume siku ya Pentekoste, bado unavutia hata siku za leo kwa kina Baba na kina Mama na zinawasukuma kutangaza Habari Njema kwa sauti ya juu maajabu ya wokovu wa Mungu katika sehemu na mazingira tofauti. Mwanzilishi alitaka kutuonyesha shauku hiyo ya mitume wa kwanza haijafa bado, na moto uliowashwa na Kristo hauwezi kuzimwa. Tamko lifuatalo lilikuwa na umuhimu wa pekee kwa Fransisi Jordani miaka ambayo kazi yake ilikuwa ikipanuka: "Nendeni kwa jina la Aliye Juu na muwaangazie wote" (SD II/21). Eternal

Tunafanya ukweli uliomkamilifu wa neno la Mungu na wa imani yetu ili ufikike na watu tamaduni zote, asili yote, matabaka yote, jamii zote, mataifa yote na dini zote.

Sheria ya Familia ya Wasalvatoriani #8

Lilikuwa ni tamko lenye kutoa dira kwa shauku la umisionari ambalo lilikuwa linabubujika kutoka katika moyo wake wa mapendo kwa ulimwengu mzima. Haikuwa ni mvuto ulio baridi na ulio na mipaka, bali ni utambuzi wa kuishi katika utume wa kumtangaza Kristo, kumfanya ajulikane na kupendwa. Roho ya Yesu na mitume ni moto unaotusukuma kujifanya upya ambao ulimtaka Fransisi Jordani kuwatia moyo watu wote, wakati na mahali popote.

b) *Wokovu ni kwa ajili ya Wote (Huruma)* – Fransisi Jordani aliangalia ulimwengu kwa huruma kama vile Yesu alivyofanya. Lengo kubwa la Mwanzilishi lilikuwa ni kushirikiana na mpango wa Mungu kwa wokovu wa ulimwengu mzima. Zaidi ya kuwafikia maskini na wale waliohitaji mwanga wa Injili, utume kwa upande wake ulikusudiwa "kuongoa." Tunu za Kikristo ziendane na

utaratibu wa wakati. Zaidi ya hayo, ninaamini lengo la karama ya Fransisi Jordani ilikuwa ni kutangaza mapenzi ya Mungu kwa wote, bila kumbagua hata mmoja. Leo tunasema kwamba mfumo wa kukuza wokovu wa Mungu unatuelekeza kuwa alama ya upendo wa Mungu ambao unawaleta watu kwa pamoja katika uhusiano wa mapendo na Yeye. Mwanzilishi kila mara alionyesha utambuzi huu kupitia sala fupi kama ifuatavyo: "Ee Bwana, ningependaje ningeungana nawe kwa karibu na kuongoza mataifa yote kwako? (SD II /75) na pia "Ee Bwana Mwenyezi, jambo hili ningelitafuta! Ningetamani vipi kumwokoa kila mmoja!" (SD I/149). Vilevile, uamuzi wake wa kuwapeleka wamisionari wake wa kwanza India inaonyesha mtazamo wake wa pekee wa kulinda na kuponya watu, kwa kufanya jitihada za kuwafikia wale wanaoteseka sana. Kabla ya kuwataka wengine waishi mitazamo ya Yesu wa kutokumbagua hata mmoja kutoka katika upendo wake na bila kumnyima hata mmoja msamaha wake, Mwanzilishi alipenda kulifanya jambo hili yeye mwenyewe. Masomo ya tafakari kulimwezesha Mwanzilishi kuchukua mambo muhimu kwenye kitabu chake cha kumbukumbu kama ifuatavyo "Mtendee jirani yako kwa pendo vilevile kana kwamba unamtendea Kristo Mwenyewe" (SD I/55), na pia "Ninahisi kwamba hatuwezi tukawa na maisha ya uchaji katika ulimwengu bila kushiriki kikamilifu kwa kuwahudumia maskini (….) n.k. (SD I/105). Katika ulimwengu wenye hitaji la wokovu, kuongelea kuhusu Yesu Kristo unatusaidia kuelewa kwa msingi mahitaji ya maskini, kwa sababu kuwaonea huruma kikamilifu ni kiini cha ujumbe wa Yesu. Papa Fransisi alisema kwamba *"…kama tukiwaondoa maskini kutoka katika Injili, hatutaweza kuelewa ujumbe wote wa Yesu Kristo".*[11] Jambo hili linalohusiana na huruma kwa ajili ya maskini, ambalo pia Mwanzilishi aliligusia, linatugusa pia sisi, Wasalvatoriani wanaume na wanawake na unatusukuma kutoa ushuhuda, kuwa alama za maisha na tumaini katika ulimwengu ulioharibika.

c) *Kubeba Msalaba kila Siku* - Haikuwa ni kwa bahati mbaya Fransisi Jordani kuchukua jina la kitawa "wa msalaba" (SD I/168) siku ya Jumapili ya Matawi, Machi 11, 1883. Jina hili ni zaidi ya cheo cha kiibada. Maandiko yake yana utenzi unaoelezea neno "wa msalaba" ina maana gani kwake. Msalaba ulikuwa ni maisha ya Mwanzilishi, wokovu wake, taji lake, utukufu wake, tumaini lake, ngao yake, ulinzi wake, urithi wake na furaha yake. Kama hitimisho katika utenzi, anaongeza "Nisijivunie kitu chochote kile ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo!" (SD I/179). Alithibitisha jambo hili miaka ya baadae kwa maneno yafuatayo: "Ee Msalaba! Ee Msalaba mtamu! Ee Msalaba! Ee Msalaba ninaotakiwa kukupenda na kujitoa zaidi sana kwa ajili ya Yesu!" (SD I/208). Kwa hiyo, msalaba ni jambo muhimu sana katika maisha ya Jordani na pia katika maisha yake ya kiroho mpaka tunasikia kwamba tunachukulia kama jambo la kawaida. Hakuna maisha ya kiroho ya wasalvatoriani yanayowezekana bila ya msalaba. Kifo cha Yesu msalabani haikuwa ni tukio linalojitenga na historia ya Jordani, bali ni ukweli unaotoa ufupisho na wajibu wa maisha yake na utume wake wote. Zaidi ya hayo, kumfuata Kristo si swala la kinadharia na kufikirika kwa mwanzilishi wetu. Kwa Fransisi Jordani, kuwa mfuasi wa Kristo kulimaanisha kujitoa uhai wake bila kujibakiza chochote, kuwa tayari kuondoa magumu yote ili kupata ulimwengu ulio mwema na Kanisa la huduma. Hakujaribu tu kuleta maana ya mateso ya siku kwa siku bali aliamini ya kwamba "Kazi ya Mungu inakuwa katika kimvuli cha msalaba" (SD I/163) na (SD II/73). Kama tunavyofahamu, alizoea kuwakabidhi msalaba wamisionari alipokuwa akiwatuma, akiwasihi kumtangaza "Yesu Msulibiwa."[12] Kwa kupitia tendo hili, Fransisi Jordani alijaribu kuwafanya vijana na mabinti zake kuelewa kwamba msalaba kwa undani wake ni mali ya wafuasi wa Kristo. Msalaba kwa ajili yetu, kutokana na Mwanzilishi, ni alama inayoendeleza

[11] *Rej. Homilia ya Papa Fransisi, Jimbo la Manila, Ufilipino (Jan. 16, 2015).*

[12] *Rej. Mawaidha ya Fransisi Jordani kwa Mkutano Mkuu, Januari 17, 1890.*

kazi ya upendo wa Mungu ambao unatukaribisha na kuwajibisha maisha yetu kwa Kristo Mwokozi, ukitukaribisha kufuata mfano wake na kuwahudumia wale wote wanaoteseka katika ulimwengu wa leo.

HITIMISHO

Upendo mkubwa wa Mwokozi wa ulimwengu ni sura inayotawala katika maisha ya kiroho ya Jordani. Aliamua kumleta Yesu Kristo kuwa kiini cha maisha yetu. Kutoka katika kumwungama Kristo kwa mazoea na kufanya nae uhusiano mpya, wa ndani kabisa na ulio hai, ambao ni wajibu tulionao kwa siku za leo, uhusiano huu ulio hai na Yesu zinakua katika maisha yetu yote. Kama tunavyoona, safari ya Fransisi Jordani kwa kufuata hatua za Yesu inaonyesha kuchukua hatua halisi ya imani, kuachana na wasiwasi na vikwazo, mpaka tutakapogundua kwamba hakuna awezae kutoa majibu ya maswali yetu ya ndani kama yeye.

Hatua ya kiroho ya Fransisi Jordani inatuwezesha kutoka ushiriki mfu tuliorithi kuelekea maisha ya kiroho ya wafuasi wa Kristo ambao umetolewa kwa ajili ya ufalme. Kwa hiyo, imani yetu isizaliwe na desturi za zamani wala kuchukua mitindo ya kisasa. Ni lazima iwe mwitiko mpya wa Injili kama tunavyosoma kupitia lensi ya maswali, mateso, furaha na matarajio ya wakati wetu. Kutokana na hili, safari ya Mwanzilishi ya imani inatuita kufanya mabadiliko, kuwa hatua ya kujifunza, kufanya mahojiano hai na ya karibu na Yesu Kristo na kuchukua upendo wake kwa ajili ya kuhubiri.

Ni lazima kuongeza kwamba utume wa Wasalvatoriani hauna uhai bila kuwa na maisha ya kiroho yaliyojengeka katika Ukristo (Christocentric). Kumfahamu Yesu Kristo na ujumbe wake wa wokovu, na wakati huohuo kumfanya ajulikane na watu wote, ni mambo mawili muhimu kwa maisha yetu ya kiroho ya kisalvatoriani. Yanaenda kwa pamoja. Maisha ya kiroho ya Wasalvatoriani yatakuwa yana uhalisia kama yatatuongoza kuelekea katika majitoleo yetu ya kitume. Zaidi ya hayo, kazi ya kitume ambayo haistawishwi na uhusiano wetu na Kristo Mwokozi haitaeleweka kamwe. Kuweka pamoja uzoefu wetu wa Kimungu (kumjua Mungu wa Yesu Kristo) na utume wetu wa kuhubiri (kumfanya Kristo na ujumbe wake ufahamike) ni muhimu na haukwepeki kama tunataka kuondoa udhaifu wa kiroho unaotusumbua kwa siku ya leo. Kutokana na Mwanzilishi wetu, kuwafanya watu wamjue Yesu Kristo vema na kumpenda Yeye kila wakati ni tunu iliyo bora sana ambayo tunaweza tukaitoa ulimwenguni. Kwa upande wetu Wasalvatoriani, kujua, kumpenda, na kumtangaza Mwokozi ni kama mapigo yetu ya moyo, kama hewa tunayovuta. Maisha yetu yanaboreshwa na kukuzwa kwa Yesu Kristo. Kwa kweli, kabla ya kwenda Roma kuanzisha jamii ya kitume, Fransisi Jordani alistaajabu: "Unaweza kupumzika wapi kama si kwa Kristo?" (SD I/145). Na, katika muda wake wa mwisho, katika hospitali ndogo huko Tafers (Switzerland), akiwa amedhoofishwa sana na ugonjwa na alikuwa karibu akipata mapumziko, maneno ya mwisho ya Fransisi Jordani inaonyesha mahusiano yake na Yesu yalikuwa ni ufunguo wa msingi na uchaguzi wa pekee wa maisha yake. Kati ya misemo inayotia moyo, inayoonyesha shukrani na msamaha, alirudia polepole sana sala ifuatayo kwa Yule ambaye alikuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yake yote:

"Ee Yesu, nakupenda! Ee Yesu, nakupenda! (...)
Yesu wangu, Mimi ni wako! Mimi ni wako, mimi ni wako tu!
Ee Yesu!![13]

---

[13] *Angalia maneno ya mwisho ya Mwanzilishi wetu yaliyonukuliwa na P. Pfeiffer kati ya Agusti 26 na Septemba 7, 1918.*

Maswali ya Tafakari

1. Soma tena Sheria za Familia ya Kisalvatoriani kwa mwanga wa makala hii.
    a. Onyesha maneno au misemo ambayo inakugusa na ujiulize, “jambo hili linaniambia mimi nini na nitalipa mwitikio gani?”
    b. Manufaa yake yanaweza kuwa ni yapi katika familia ya Kisalvatoriani katika eneo lako la ulimwengu au/na kwa ulimwengu mzima?
2. Kwa mwanga wa makala hii, kama ukiamua kuitengeneza upya sheria ya familia ya Wasalvatoriani, Je, Utaongeza kitu gani au kukibadili?
3. Jinsi gani unapata utambuzi na mwangaza wa Msalvatoriani katika mitume kutoka uhusiano wa pekee wa Baba Jordani na Yesu, Mwokozi wake?